



## **BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

### **ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

#### **BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI**

#### **MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Nane – Tarehe 16 Februari, 2018.**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua itasomwa.

#### **I. TAARIFA YA SPIKA:**

#### **II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

##### **Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2017/2018.

#### **III. MASWALI:**

##### **Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

45. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa Programu ya usimamizi na utumishi wa Idara Maalum za SMZ moja kati ya majukumu yake ni kutoa miongozo ya ajira, kupandisha vyeo na kuongeza muda wa utumishi, na kwa sababu wapo Askari ambao wameshakwenda kwenye kozi mbali

mbali tokea 2014 na hadi leo bado hawajapandishwa vyeo kwa mujibu wa kozi walizosomea.

- (a) Je, ni lini Askari na maafisa ambao wameshamaliza kozi watapandishwa vyeo vyao.
- (b) Je, ni watumishi wangapi waliomaliza muda wao wa kazi waliongezwa muda na fani zao ni zipi.
- (c) Je, mtu ambae alistaafu na akapewa mkataba wa muda wa miaka miwili anastahiki kuongezwa muda kama huo mara ngapi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

**Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:**

- 39 MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

Kwenye hotuba ya Bajeti ya mwaka 2016/2017 Waziri wa Wizara hiyo alieleza kwamba Serikali imeanzisha mpango wa utambuzi wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu, kwa shehia mbali mbali za Unguja na Pemba jambo ambalo linaweza kuleta mafanikio makubwa ya kupunguza idadi ya watoto wanaozurura ovyo mitaani na kutumikishwa kwa malipo madogo.

- (a) Je, baada ya kuwatambua vijana hao Serikali imechukua hatua gani za kuzisaidia familia zenye watoto hao ili kuepukana na kuishi katika mazingira magumu ambayo wanaishi nayo hivi sasa.
- (b) Je, ni familia na watoto wangapi ambao wapo kwenye familia zinazoishi katika mazingira magumu kwa shehia zilizofanyiwa uchambuzi kwa Unguja na Pemba.

- (c) Je ni utaratibu upi unaotumika kuzitambua familia hizo hadi kufikia Novemba, 2017 ni familia ngapi zimeshatambuliwa.

**Wizara ya Afya:**

33. MHESHIMIWA SIMAI MOH'D SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya.

Katika utekelezaji wa Ilani ya CCM 2015 – 2020, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliahidi kujenga hospitali Binguni.

- (a) Je, ni hatua gani ambazo zimefikiwa hadi hivi sasa.
- (b) Ni utaratibu upi utakaotumika na Wizara ya Afya kuhakikisha ajira zitakazotoka na ujenzi huo zitawanufaisha wananchi wa eneo husika hasa maeneo ya Dunga, Mtakuja, Binguni na Tunguu.

**Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:**

8. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Kwa kuwa Wizara ina Programu ndogo ya upangaji wa matumizi bora ya Ardhi. Na kwa sababu maeneo ya Kombeni, Kisakasa, Dimani, Nyamazi hadi Fumba ni maeneo ambayo ujenzi wake ni wa kisasa lakini bado kuna tatizo la kujenga majumba bila ya kufuata mpango bora wa upangaji wa miji .

- (a) Je, Wizara ina mpango gani wa kusimamia ujenzi kwa maeneo hayo ili kuhakikisha kwamba maeneo hayo yamepimwa na ili watu waweze kujenga nyumba zao kwa mujibu wa maelekezo ya upangaji bora wa mji ili kuepuka ujenzi holela kwa maeneo hayo
- (b) Je, Wataalamu katika sekta ya upangaji wa matumizi bora ya ardhi wana utaratibu wa kuyakagua maeneo hayo ili kutoa taaluma za aina ya ujenzi na upangaji wa miji kwa eneo

hilo ukitilia maanani kwamba maeneo mengi ya huko yanajengwa miji mikubwa ya kisasa.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:**

26. MHESHIMIWA SIMAI MOH'D SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Katika majumuisho ya bajeti ya mwaka 2017/2018, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ilijipanga kupata mshauri ili kuondoa kero kwa wanachi wa kisiwa cha Uzi katika kuimarisha barabara ya kutoka Unguja Ukuu kupitia kwenye mikoko kuelekea Uzi.

Ni hatua gani zimefikiwa na hadi sasa ni maamuzi yapi yamechukuliwa na Serikali.

**IV. HOJA ZA KAMATI:**

**Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:**

Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2017/2018.

Zanzibar,  
16 Februari, 2018.

(Raya Issa Msellem)  
**KATIBU WA BARAZA.**